

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI DIRMA,  
S.L.P 256,  
KATESH – HANANG. 20/11/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DIRMA

### 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021 shule ya sekondari Dirma iliyopo katika Kata ya Dirma. Muhula wa kwanza masomo yanaanza tarehe 17.01.2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 17.01.2021 hadi 21.01.2021.

### 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA .

2.1. SARE ZA SHULE ❖ Sare ya shule hii ni suruali Khaki shati nyeupe kwa wavulana na sketi ya khaki) blauzi nyeupe kwa wasichana.

❖ Rangi ya hijab ifanane na sare za shule(blauzi).

2.2MAELEZO: ❖ SKETI> Khaki marinda 12, mkanda wa wastani. Pair 02. Pindo la chini wastani lisiwe dogo.

❖ SURUA khaki mifuko ya pembeni “V” yenye kifungo mfuko wa nyuma – pair 2 kwa wavulana wote.

❖ VIATU> vyeusi vya kamba, visigino vifupi (wote) – pair 2

❖ SOCKSI> Khaki (Wavulana, nyeupe (wasichana) – pair 2

❖ SWETA> damu ya mzee (wasichana) na (wavulana) shingo V iliyopimwa vema pair 2 (wote).

❖ Sare ya michezo kwa shule hii ni raba, Trucksuti ya Blue (ni lazima)

- ❖ Wavulana raba T – shirt ya kijani – pair 2
- ❖ Wasichana raba, T – shirt ya blue – pair 2

2.2 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu, counter books kwa masomo yote 9 na sio madaftari madogo (hayaruhusiwi) na rimu paper 1 (A4) kwa mwaka zisiwe za mistari (ni muhimu sana kwa ajili ya kufanyia mitihani).

2.3 Chakula cha wanafunzi wa kutwa mahindi debe 3 kwa mwaka , maharage debe 2 kwa mwaka na Tshs. 73000/= kwa mwaka.

2.4 Vifaa vya usafi; mwanafunzi aje na ufagio wa chelewa, ndoo ya lita kumi na jembe.

**MUHIMU: 1. IKIWA MWANAO ANALOTATIZO LA KIAFYA UJE NA TAARIFA**

**TOKA KWA DAKTARI.**

**2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE UTAZIKUTA KATIKA MBAO ZA SHULE.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

.....

ROGATHE B. MUNISI

MKUU WA SHULE